*Tafsiri hii imefanywa na Social Development Direct na Shirika la Translators without Borders kwa lengo la kufahamisha tu. Muungano wa Mashirika ya Uingereza yanayofanya kazi katika Maendeleo ya Kimataifa (BOND) hauwezi kuthibitisha usahihi wake. Toleo rasmi la pekee lililoandikwa kwa Kiingereza linaweza kupatikana kwenye wavuti wa BOND [*[Safeguarding policy templates | Bond](Safeguarding policy templates | Bond)*].'*

# Kanuni za Maadili za Kulinda Usalama za BOND

## Utangulizi

Katika kudumisha maono na maadili yake, [Shirika lisilo la Kiserikali (NGO)] limejitolea kudumisha kiwango cha juu sana cha maadili miongoni mwa wafanyakazi wake wote na watumishi wanaohusiana nao. Ili kusaidia kuboresha uelewa, Kanuni hizi za Maadili zinafafanua kwa kina matarajio ya [Shirika lisilo la Kiserikali] ya wafanyakazi katika maeneo muhimu.

## Upeo na lengo

Kanuni hizi za Maadili zinawahusu wafanyakazi wote wa mikataba, wa kimataifa na wa ndani, walioajiriwa na [Shirika lisilo la Kiserikali]. Kanuni za Maadili zilizorekebishwa zinatumika kwa wafanyakazi wakujitolea, washirika, wanakandarasi na wauzaji.

Lengo la Kanuni hizi za Maadili ni kuweka bayana mwenendo unaotarajiwa wa wafanyakazi wa [Shirika lisilo la Kiserikali], wanapokuwa na mkataba na shirika, na zinakuwa sehemu ya mikataba yote ya ajira. Kanuni hizi za Maadili zinatumika wakati wote. Ukiukwaji wa Kanuni za Maadili ni msingi wa kuchukuliwa hatua za kinidhamu, hadi kujumuisha kuachishwa kazi.

Huku tukitambua kuwa sheria na tamaduni za ndani zinatofautiana pakubwa kutoka nchi moja hadi nyingine, [Shirika lisilo la Kiserikali] ni Shirika la Kimataifa lisilo la Kiserikali, kwa hivyo Kanuni za Maadili zimetungwa kutokana na viwango vya kimataifa na vya Umoja wa Mataifa. Wafanyakazi wa [Shirika lisilo la Kiserikali] wanatarajiwa kuzingatia sheria za mahali popote wanapofanya kazi, isipokuwa pale ambapo Kanuni za Maadili ni kali sana, kwa hali hiyo Kanuni hizi zitumika.

## Dhamira na maadili

[Ingiza Taarifa ya Dhamira ya Shirika lisilo la Kiserikali au Maadili ya Shirika hapa]

*Shukrani kwa Shirikisho la CHS*

# Viwango vya Kanuni za Maadili

Mimi kama mfanyakazi wa [Shirika lisilo la Kiserikali]:

**Nitadumisha uadilifu na sifa za [Shirika lisilo la Kiserikali] kwa kuhakikisha kuwa mwenendo wangu wa kitaaluma na wa kibinafsi unawiiana na maadili na viwango vya [Shirika lisilo la Kiserikali]**

- Nitawatendea watu wote haki kwa heshima na utu
- Wakati wa kufanya kazi katika muktadha wa kimataifa au kusafiri kimataifa kwa niaba ya [Shirika lisilo la Kiserikali], nitazingatia sheria zote za ndani na kuwa mwangalifu kwa desturi za wenyeji
- Nitahakikisha kuwa mwenendo wangu hauliingizi [Shirika lisilo la Kiserikali] katika sifa mbaya na hauathiri au kudhoofisha uwezo wangu wa kutekeleza jukumu langu kama mwajiriwa
- Sitafanya kazi chini ya ushawishi wa pombe au matumizi, au kuwa na, dawa za kulevya kwenye majengo au makazi ya [Shirika lisilo la Kiserikali]

**Sitajihusisha na mwenendo wa dhuluma au unyonyaji**

- Sitahusika katika tendo la ngono na watoto (watu walio chini ya umri wa miaka 18). Huwezi kutumia kutojua umri wa mtoto kujitetea
- Sitabadilisha pesa, ajira, bidhaa, au huduma kwa ngono, ikijumuisha mapendeleo ya kingono au aina zingine za tabia ya kudunisha, kudhalilisha au tabia ya unyonyaji, zimepigwa marufuku. Tabia hizo zinajumuisha ubadilishaji wowote wa msaada unaokusudiwa kuwafikia wanaofaidika kwa msaada
- Sitashiriki katika mahusiano ya kingono na wanaofaidika kwa msaada, kwani mahusiano kama hayo yanahusu mamlaka yasiyo sawa
- Sitashiriki katika shughuli zozote za kibiashara za kiunyonyaji na watoto au watu wazima walio katika hali hatarishi ikiwemo ajira ya watoto au usafirishaji haramu
- Sitamdhulumu kimwili mtoto au mtu mzima aliye katika hali hatarishi
- Sitamnyanyasa kihisia au kisaikolojia mtoto au mtu mzima aliye katika hali hatarishi

**Nitahakikisha usalama, afya na ustawi wa wafanyakazi wote wa [Shirika lisilo la Kiserikali] na wafanyakazi wote wanaohusishwa (wafanyakazi wa kujitolea, washirika, wauzaji na wanakandarasi)**

- Nitafuata mahitaji yote ya kisheria na ya kiafya na usalama ya shirika zinazotumika katika eneo langu la kazi
- Nitafuata miongozo yoyote ya usalama ya eneo langu na kuarifu usimamizi kuhusu mabadiliko yoyote muhimu kwa miongozo hiyo
- Nitaenenda kwa namna inayoepuka hatari yoyote isiyofaa kwa usalama, afya na ustawi wangu na wengine, ikiwemo mashirika yanayoshiriki nasi na jamii tunazofanya kazi nazo

**Kuwajibika kwa matumizi ya habari, mali na rasilimali ambazo nazifikia kwa sababu ya kuajiriwa na [Shirika lisilo la Kiserikali]**

- Nitahakikisha kuwa natumia mali na rasilimali za [Shirika lisilo la Kiserikali] nilizokabidhiwa kwa njia ya uwajibikaji na nitatoa hesabu za pesa na mali yote
- Sitatumia vifaa vya [Shirika lisilo la Kiserikali] vya Teknolojia ya Habari, programu au baruapepe na majukwaa ya mitandao ya kijamii kushiriki katika shughuli ambazo ni haramu chini ya sheria za ndani au za kimataifa au zinazohimiza mwenendo ambao unaweza kuwa kosa la jinai. Hii

inajumuisha nyenzo yoyote inayohujumu au kunyanyasa kundi lolote kwa msingi wa sifa zilizolindwa, au kuhimiza msimamo mkali
- Sitatumia vifaa vya [Shirika lisilo la Kiserikali] vya Teknolojia ya Habari kutazama, kupakua, kubuni, kusambaza au kuhifadhi katika muundo wowote nyenzo zisizofaa au za kudhulumu ikijumuisha sio tu ponografia au kuonyesha dhuluma ya watoto

**Nitafanya kazi zangu na kuishi maisha yangu binafsi kwa njia ambayo inaepuka migongano ya maslahi**

- Nitaweka wazi maslahi yoyote ya kifedha, ya kibinafsi, au ya familia (au ya uhusiano wa karibu sana) katika masuala ya biashara rasmi ambayo yanaweza kuathiri kazi ya [Shirika lisilo la Kiserikali]
- Sitahusika katika kumpa faida, mikataba ya bidhaa au huduma, ajira, au kuendeleza katika [Shirika lisilo la Kiserikali], mtu yeyote ambaye nina maslahi naye ya kifedha, ya kibinafsi, ya kifamilia (au uhusiano wa karibu sana)
- Nitaomba ruhusa kabla ya kukubali kuteuliwa kama mgombeaji anayetarajiwa au jukumu lingine rasmi katika chama chochote cha siasa
- Sitakubali zawadi kubwa au malipo yoyote kutoka kwa serikali, jamii ambazo tunafanya kazi nazo, wafadhili, wauzaji na watu wengine ambazo ninazopatiwa kutokana na ajira yangu na [Shirika lisilo la Kiserikali]

**Kudumisha usiri**

- Nitakuwa mwangalifu ipasavyo katika masuala yote ya biashara rasmi, na kutotoa taarifa yoyote ya siri inayohusiana na wafanyakazi wenzangu, masuala yanayohusiana na kazi au habari yoyote nyeti isipokuwa ikihitajika kisheria kufanya hivyo

# Malalamishi na ripoti

Wafanyakazi wa [Shirika lisilo la Kiserikali] wanawajibu wa kumjulisha msimamizi husika tukio lolote linaloweza kutokea, dhuluma au kero ambazo wanashuhudia, wanajulishwa, au wanashuku linaloonekana kukiuka Viwango vilivyomo katika Kanuni za Maadili. Wafanyakazi wa [Shirika lisilo la Kiserikali] wanaoripoti kero wanalindwa na sera ya Kufichua Matendo yasiyofaa Mahali pa Kazi.

Wafanyakazi ambao wana malalamishi au kero zinazohusiana na ukiukwaji wa Kanuni za Maadili wanapaswa kutoa kuripoti mara moja kwa Meneja wao. Ikiwa mfanyakazi hahisi vizuri kutoa kuripoti kwa meneja wake (kwa mfano ikiwa wanahisi kutoa ripoti hiyo haitachukuliwa kwa uzito, au ikiwa msimamizi huyo anahusika na kero hiyo) anaweza kutoa kuripoti kwa mfanyakazi mwingine yeyote anayefaa. Kwa mfano, huyu anaweza kuwa msimamizi mkuu au mmoja wa Timu ya Rasilimali Watu.

Wafanyakazi wanaopokea ripoti au kero wanalazimika kuchukua hatua au kuipeleka mbele ripoti hiyo mara moja kulingana na Sera ya Malalamishi na Taratibu za [Shirika lisilo la Kiserikali]

# Sera zingine zinazohusika

Sera ya Malalamishi na Taratibu

*Shukrani kwa Shirikisho la CHS*

Sera ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi

Sera ya Kufichua Matendo yasiyofaa Mahali pa Kazi

Sera ya Kupambana na Udanganyifu na Ufisadi

Sera ya kulinda usalama

Sera ya Kupambana na Uonevu na Unyanyasaji

Sera ya usalama

Sera ya matumizi ya Teknolojia ya Habari

---

Kwa kukubali ajira naahidi kutekeleza majukumu yangu na kudhibiti mwenendo wangu kulingana na mahitaji ya Kanuni ya Maadili

Jina:

Saini:

Tarehe: